# Uponyaji

## Healing

Katika Yohana sura ya 5 msitari wa 19 na 20 tunasoma kile Yesu alisema, kwa wale walio mkosoa kwa kuwa waponya wagonjwa katika siku ya Sabato. Alikuwa amemponya mtu katika bawa la Bethzatha na ikawa ni siku ya Sabato wakati aliufanya mujiza huu. "Yesu akajibu akawa ambia amini nawaambieni mwana hawezi neno mwenyewe ila lile amwona Baba analitenda,

Kwa maana yote ayatendayo yeye, ndiyo ayatendayo mwana vile vile. Kwakuwa Baba ampenda mwana, naye amwonyesha yote ayatendayo mwenyewe, hata na kazi kubwa kuliko hizi atamwonyesha ili ninyi mpate kustaajabu." Yesu hangeweza kumwekea mtu yeyote mkono au kuamrisha uponyaji wowote isipokuwa ameagizwa na Baba kufanya hivyo.

Katika Kutoka sura ya 40 msitari wa 36 hadi 38, tunasoma kuhusu wingu lililokuwa juu ya hema ya kukutania ambalo liliwafuata Musa pamoja na watumwa wa awali wa Kihebrania kupitia jangwani. "Na hapo lile wingu lilipoinuliwa kutoka juu ya maskani wana wa Israeli wakaenda mbele katika safari zao zote, bali kama lile wingu halikuinuliwa, wakati ule hawakusafiri hata siku ile lilipoinuliwa tena.

Kwa maana lile wingu la Bwana lilikuwa juu ya maskani wakati wa mchana, na kulikuwa na moto ndani yake wakati wa usiku, mbele ya macho ya nyumba ya Israeli katika safari zao zote." Hata katika miaka hiyo ya maelfu iliyopita Bwana alikuwa anajaribu kuwafundisha watu wake somo la thamana – "msisonge mpaka nitakapo songa."Historia ya kanisa ingelikuwa tofauti kabisa iwapo kanisa litasoma somo hili la thamana sana.

Kumwekea mtu mikono ni imani pekee iwapo Mungu ameamrisha iwezekufanyika kwa wakati huo, Paulo anaandika katika Warumi sura ya 10 msitari wa 17: "Basi imani chanzo chake ni kusikia, na kusikia huja kwa neno la Kristo." Basi iwapo tutaweka mikono juu ya mtu na tuombee uponyaji wao pasipo kuelekezwa na Mungu, kile tunachofanya sio katika imani ni kutoka kwa akili zetu wenyewe, labda ndio sababu hakuna uponyaji mwingi katika makanisa ya mataifa ya magharibi.

Katika Luka sura ya 17 msitari wa 17, tusoma kitu cha manufaa sana katika somo hili. "Ikawa siku zile moja yapo alikuwa akifundisha, na Mafarisayo na waalimu watorati walikuwa wameketi hapo, waliotoka katika kila kijiji cha Galilaya, na Uyahudi, na Yerusalemu, na uwepo wa Bwana ulikuwepo apate kuponya."

Kifungu hiki kinapendeza sana kwa sababu katika lugha ya kiingerrza hakuna taarifa ya kadri. Iwapo tunasoma kuwa nahodha wa meli alikuwa imara siku hiyo inaoyesha kuwa kulikuwa na wakati mwingi ambao hakuwa. Sawa na msitari huu kutoka kwa injili ya Luka kweli kuwa inasema "nguvu za Bwana zilikuwepo kuponya" inaweza kuonyesha kuwa hili halikuwa hivyo kila mara.

Tushaona kuwa Yesu hangefanya chochote chake binafsi lakini kile ambacho Baba alikuwa anafanya, basi lazima tulizingatie hilo tunapoita mkutano ilikuwaombea, watu wanaohitaji uponyaji iwapo nguvu za Bwana sitakuwepo kuponya katika tukio hilo, au itakuwa Baba hatakuwa akifanya uponyaji sana katika tukio hilo? Hebu tuangalie tena katika sehemu nyingine inayopendeza sana ya Yohana sura ya 5, inayotuambia nini kilifanyika kabla ya misitari ambayo tumekuwa tukiiangalia. Msitari ni 1hadi 13 na imenukuliwa hapo chini.

"Na hapa palikuwa na mtu, ambaye alikuwa hawezi muda wa miaka thelathini na minane. Yesu alipomwona huyu amelala, naye akijua amekuwa hali hiyo siku nyingi alimwambia, wataka kuwa mzima? Yule mgonjwa akamjibu Bwana, mimi sina mtu wakuniweka birikani, maji yanapotibuliwa, ila waklati ninapokuja mimi, mtu mwingine hushuka mbele yangu.

Yesu akamwambia simama ujitwike gondoro lako, uende mara yule mtu akawa mzima, akajitwika, gondoro lake akaenda.. Nayo ilikuwa ni siku ya Sabato. Kwa sababu hiyo Wayahudi wakamwambia yule aliyeponywa, leo ni Sabato, wala si halali kwako kujitwika gondoro. Yeye aliyenifanya kuwa mzima ndiye aliyeniambia jitwike gondoro lako uende.

Basi wakamwuliza, yule aliye kuambia jitwike ni nani? Lakini yule mtu aliyeponywa hakumjua ni nani, maana Yesu alikuwa amejitenga, kwa sababu palikuwa na watu wengi mahali pale." Iwapo tutakuwa waaminifu kwetu wenyewe na Mungu, kunao wakristo wachache ambao hawataweza, wakiwa wameona muujiza mkubwa kama huo umefanyika wakati wamemwombea mtu, wanaenda saa hiyo hiyo na kuombea kila mtu aliye mahali hapo.

Tukijua kuwa Yesu ni wa rehema, je, ni kwanini hakufanya hivi? Jibu laweza kuwa ni kwa sababu bila shaka Baba hakumwambia hafanye hivyo, Alimwambia amwombee huyo mtu mmoja pekee, akiwa amefanya hivyo kwa utiifu Yesu anatoka hapo kwa ghafla.

Je, ulitambua kuwa wakati watu wale vipofu walipokuja kwa Yesu ilikupokea kuona kwao, Yesu aliwaponya kwa njia tatu tofauti? Ya kwanza tutaangalia katika hadithi hii ya Batimayo inayopatikana katika Marko sura ya 10 msitari wa 46 hadi 52. Inasema hivi: "Wakafika Yeriko: Hata aliposhika njia kutoka Yeriko, pamoja na wanafunzi wake, na mkutano mkubwa, mwana wa Timayo batimayo yule mwombaji kipofu alikuwa ameketi kando ya njia.

Naye aliposikia ya kwamba ni Yesu Mnazareti, alianza kupaza sauti yake akisema mwana wa Daudi Yesu unirehemu. Na wengi wakamkemea anyamaze, lakini alizidi kupaza sauti, mwana wa Daudi unirehemu. Yesu akasimama akasema, mwiteni.

Wakamwita yule kipofu wakamwambia jipe moyo inuka, anakuita. Akatupa vazi lake, akaruka, akamwendea Yesu. Yesu akajibu akamwambia, wataka nikufanyie nini? Yule kipofu akamwambia, Mwalimu wangu nataka nipate kuona. Yesu akamwambia enenda zako, imani yako imekuponya. Mara akapata kuona, akamfuata njiani."

Katika Yohana sura ya 9 ni njia tofauti kwa pamoja. Msatari wa 1 hadi 7 unaelezea hadithi. "Hata alipokuwa akipita alimwona mtu kipofu tangu kuzaliwa. Wanafunzi wake wakamwuliza, wakisema Rabii, ni yupi aliyetenda dhambi, mtu huyu au wazazi wake, hata azaliwe kipofu? Yesu akajibu huyu hakutenda dhambi, wala wazazi wake, bali kazi za Mungu zidhilihishwe ndani yake. Imetupasa kufanya kazi zake yeye aliyenipeleka maadamu ni mchana, usiku waja asipoweza mtu kufanya kazi. Mda nilipo ulimwenguni mimi ni nuru ya ulimwengu. Alipokwisha kusema hayo, alitema mate chini akafanya matope, kwa yale mate. Akampaka kibofu kope za macho, akamwambia nenda kanawe katika birika la Siloamu, (maana yake aliyetumwa). Basi akaenda na kunawa, akarudi anaona."

Tukio la tatu linapatikana katika Marko sura ya 8 msitari wa 22 hadi 25. "Wakafika Bethsaida, wakamleta kipofu, wakamsihi amguse, Akamshika mkono yule kipofu, akamjukua nje ya kijiji, akamtemea mate ya macho, akamwekea mikono yake akamwuliza, waona kitu?

Akatazama juu akasema, naona watu kama miti, inakwenda. Ndipo akaweka mikono yake, juu ya macho yake, naye akatazama sana, akawa mzima, akaona vyote waziwazi." Unafikiria ni kwanini Yesu aliwaponya watu hawa vipofu kwa njia tofauti? Je ni kuonyesha kuwa anapenda njia tofauti, au alikuwa anajifurahisha kufanya vitu tofauti kwa wakati huo?

Inauwezekano kabisa kuwa Baba alimwongoza kuwaponya watu hawa kwa njia hizi tofauti, na kwa sababu Yesu alikuwa akipokea maagizo kutoka kwa Baba aliweza kufaulu katika kila tukio. Kwa nini Yesu alimwuliza mtu yule iwapo anaona kitu? Huu ndio wakati pekee Yesu alifanya jambo kama hili, hata hivyo hili ni funzo zuri kwetu sisi.

Mtu huyo hakusema, "Sitamwacha shetani apate ushidi kwa kusema bado siwezi nikaona sawasawa, au nina ponywa kwa imani kwa hivyo nitakiri kuwa ninaona sawasawa na kila kitu kita kuwa sawa." Mtu huyu hakusema chochote kati ya mambo haya. Alikuwa wazi kwa Yesu na kumwambia hali jinsi ilivyo na sio vile angeitaka kuwa.

Si ni kweli kuwa, wakati mwingine tunakuwa kiroho sana, mpaka kiburi hakituruhusu kuwa waminifu na kukubali udhaifu wetu aidha kwa ndugu zetu na dada zetu katika Kristo, au kwa Mungu. Kwa sababu mtu huyu alikuwa mwanifu kwa Mungu aliona kazi imekamilika, iwapo angekuwa na kiburi na kiroho sana angekuwa anawaona watu milele kama miti inatembea. Iwapo hatutaki kuwa waminifu kwa ndugu zetu na dada zetu katika Kristo, basi wacha tuwe waminifu kwa Mungu.

Je, umewahi kutambua jinsi watu wengine watakuja mbele kwa ajili ya maombi, na inaonekana kana kwamba wamepokea uponyaji wao, na mwezi unaofuatia wanarudi kuomba maombi tena kwa ajili ya ugonjwa huo huo au shida ile ile? Iwapo hauna maelezo ya sababu hiyo ni kuwa, umekuwa ukiombea dalili badala ya kiini kinacho sababisha.

Iwapoutavunja kichwa cha magugu shambani mwako, unaweza tambua kuwa inamea tena kwa haraka, hii ndiyo sababu tunapowaombea watu uponyaji tunastahili kupambana na kiini, na sio tu dalili. Kuna magonjwa mengi ambayo yalikuja kama uridhi kutoka kwa mababu zetu.

Iwapokuna mtu katika familia kwa wakati mmoja alikuwa mlevi, inawezekana wewe pia ukawa katika umri Fulani maishani mwako. Kuna mtu yeyote katika familia yenu aliyejitoa uhai wake? Iwapo yupo kweli ni kuwa kama haitavunjwa katika ulimwengu wa roho, kuna uwezekano wako kufanya hivyo kama hata vile ulivyo.

Kuna mambo mengi ambayo yanafanana na magonjwa na ulevi yaliotajwa hapo chini, ni orodha inayochosha, mifano micheche tu: Magonjwa yanayohusiana na uvutaji wa sigara, kansa, msukumo wa damu, ugonjwa wa akili, umaskini, unyogovu na pamoja na mambo mengi mengine.

Watu wengi usema kuwa sababu kamilifu imefika (Yesu) hatuhitaji neno la maarifa, utambuzi au vingine vingi vipawa vya Roho Mtakatifu vilio orodheshwa, lakini unapokuwa unawaombea wagonjwa mwuulize Mungu akuonyeshe kiini cha shida yao, katika matukio mengi atakuonyesha, ndipo utaomba na matokeo mengi kuonekana.

Watu wengi huliza ni kwa nini Mungu anaruhusu magonjwa baada ya kifo cha Yesu msalabani, na hata ufufuo wake, lakini twaweza kuona kutoka kwa maandiko kuwa magonjwa yote yanaweza kufatwa nyuma mpaka wakati Adamu na Hawa walipomwasi Mungu, na basi dhambi na magonjwa yakaingia ulimwenguni. Swali la halali ni "Kwanini tunaruhusu dhambi katika ulimwengu ambao Yesu ametuamru tuweze kuutawala kwa jina lake?

Unahitaji kutembea tu katika barabara za mji wako mwenyewe, ili uweze kutambua mambo mengi tofauti ambayo yanaendelea katika taifa lako, pasipo mtu kuchukua hatua na kuzuia dhambi hizi kuendelea. Kulikuwa na mtu miaka iliyopita, aliyelazwa hospitalini kwa kuvimba kiambatisho. Hakuweza kuelewa ni kwa nini Mungu anaweza kurusu hili kufanyika kwake baada ya kuwa amemtumkia Bwana kwa miaka mingi, kweli kutoka ujanani mwake.

Alilazwa haraka hospitarini na baada ya upasuaji alikuwa na nafasi ya kuongea na watu wengine, kuhusu kile alichokuwa anapenda kuzungumzia zaidi – Yesu na injili ya kweli. Aliruhusiwa kukaa hospitarini iliapate nafuu kutokana na upasuaji, kwa wakati huo nusu ya wodi na wafanyakazi wote waliokuwa wanafanya kazi ndani ya wodi hiyo wakapokea wokovu kupitia Yesu.

Wakati Yusufu alikutana na ndugu zake baada ya siku nyingi alitoa ujubme mzito kwao. Akasema, "Lakini ninyi, mlifikira mabaya kwangu lakini Mungu aliyafanya kuwa mema, kuyaleta kuwa kama ilivyo siku ya leo, wokovu kwa watu wengi." Hutufai kusahau kamwe kuwa kuna kitu kama vita vya kiroho na hakuna kitu kama mapigano kati yako na adui.

Iwapoutakataa kumshambulia basi unajua wazi kuwa anaweza kukushambulia pasipo kujali. Hii ndio sababu tumepewa silaha zote za vita, na kwanini tusisitumie kila siku, ilikuwa tuweze kushida mishale ya mwovu. Wakati unaanza kuyaangalia mambo katika mtazamo wa kinyume shatani anafurahia, kwa sababu sasa huwezi ukamsifu Mungu, lakini unaopo msifu

Mungu anachukia hilo na hawezi akakaribia. Katika Yakobo sura ya 1 msitari wa 2 tunasoma ujumbe wa kuvuta – pumzi na pendekezo, kufanya kitu ambacho kikombali na kuwesekana kufanyika. “Ndugu zangu, hesabuni kuwa ni furaha tupu, mkiangukia majaribu mbalimbali; mkifahamu ya kuwa kujaribiwa kwa imani yenu huleta saburi.

Saburi na iwe na kazi kamilifu, mpate kuwa wakamilifu na watimilifu bila kupungukiwa na neno.” Pia kuna ahadi ya ajabu kama hiyo. Warumi sura ya 8 ms 28 inasema: “Nasi twajua kuwa katika mambo yote Mungu hufanya kazi na wale wampendao, katika kuwapa mema, yaani, wale walioitwa kwa kusudi lake.”

Wakati watumwa halisi wa Kihebrania walitoka Misri walikosa kuingia katika Nchi ya Ahadi, kwa sababu walikuwa wanalalamika kila wakati, wakiwa kinyume na wakiangalia magumu tu badala ya kumwangalia Mungu aliyekuwa na majibu mkononi Mwake kama ilivyo hakika.

Utakosa kuingia Nchi ya Ahadi iwapoutafanya hivyo pia. Mungu amefanya yote yanayohitajiika kwako kufikia ukomavu katika Kristo, na uufikie utimilifu wa kimo chake ndani ya Kristo, iwapo utafaulu au kushindwa hilo linategemea wewe. Katika 1 Wakorintho sura ya 9 msitari wa 24 hadi 27 tunasoma: “Je! Hamjui ya kuwa wale washindanao kwa kupiga mbio, hupiga mbio wote, lakini apokeaye tuzo ni mmoja? Pigeni mbio namna hiyo, ili mpate. Na kila ashindanaye kitika michezo hujizuia yote.

Basi hufanya hivyo kusudi wapokee taji iharibikayo; bali sisi tupokee taji isiyoharibika. Hata mimi napiga mbio vivyo hivyo, si kama apigaye hewa; bali na utesa mwili wangu na kuutumikisha, isiwe ni kisha kuhubiri wengine mwenyewe niwe wa kukataliwa.”

Katika usawa wote kwa kila anaye husika, lazima isemwe kuwa kuna hali nyingi ambapo mateso ya watu walio na magonjwa kunatokana na udhalimu na udanganyifu. Kwa mfano, mwaka wa 1976 kulikuwa na mtetemeko mkubwa wa ardhi Sicily kisiwa kikubwa cha magharibi mwa Italy, kutokana na mtetemeko huu watu wengi walipoteza nyumba zao, na wengi wao kama sio wote mali zao.

Pesa nyingi ziliweza kuchangwa ili kuwasaidia watu hawa kupitia wito wa kimataifa, lakini sehemu ya pesa nyingi zilizo changwa hazi kuwafikia ili kuwasaidia watu hawa, nyingi ya pesa hizi zilielekezwa kwenye akaunti za wanachama wa ‘The Mafia’ na mashirika mengine ya kigaidi. Kwa sababu ya hili watu wengi wakawa wagonjwa, kupitia magonjwa ya kuambukizana kutoka kwa maji kwa kuwa hawangeweza kupata maji safi ya kunywa, walikuwa wanakunywa chochote kilicho patikana, na kwa wakati mwingi yalikuwa yameambukizwa na maji machafu. Kutokana na hili wengi wakafa na walioepuka kifo wakawa wagonjwa sana.

Hili sio tukio pambalo limetengwa, wakati kulikuwa na michezo tofauti ya kuigiza, ulimwenguni kote, iliyopangwa na Bob Geldo kuchangiza mamilioni kwa wale waliokuwa wamekubwa na janga la njaa, mamilioni ya paundi zilipeanwa kwa mataifa tofauti ili waweze kuwalisha maskini wao, na mataifa yaliyokuwa na janga la njaa, hata hivyo tena kiasi kingi cha pesa hizi kilielekezwa kwa manufaa ya wanachama wengi wa serikali hizo, kabla kiasi chochote kupewa kwa taifa lao kwa wale waliona njaa.

Wakati matajiri wanaendelea kupata utajiri zaidi hakuna hata wazo linalopewa wale walio sehemu kama za Uganda, wengi wao ambao ni watoto yatima ambao siku nyingi wana lala bila kuweza kupata hata mlo moja kwa siku hiyo. Kwa sababu hawawezi kupata maji safi ya kunywa wana kunywa chochote wanachoweza, na hili linasababisha kuzambashwa kwa magonjwa mengi hatari kama kipindupindu.

Itatumia kama kiwango cha matumizi ya siku moja kwa usalama katika taifa la magharibi, kukomeza malaria kutoka kwa mataifa iwapo tu mataifa yatakuja pamoja, na kuchukua hatua, lakini wanachukulia kuwa hawahusiki kiuchumi kufanya hili. Magonjwa mengine yanaweza kukomeshwa kutoka ulimwenguni iwapo, wale walio katika mataifa tajiri wanaweza kuamua kuwa hili ndilo wangetaka kufanya.

Mataifa mengi hata hivyo yanafanya faida kubwa kutoka kwa mauzo ya madawa, katika mataifa ambayo magonjwa hayo yamejaa, kwa hivyo kwa wazo unaweza ona ni kwa nini wanafikiria hivyo, kinacho hitajika ni kubadilishwa kwa moyo wa mwanandamu; hili ni jambo ambalo ni Mungu pekee anayeweza kulileta, watu wengi huteseka sana kupitia vita, hivi vita pungua kabisa na hakuna yeyote atakayeachwa akiteseka kwa njaa au hata kwenda kulala bila chakula, wakati Yesu ataanza ukutawala wake wa miaka 1000

Maji safi yatapatikana kwa kila mtu bila malipo, na ulimwengu utapata kujua rehema ambazo hizijapata kuwepo katika ulimwengu huu kwa milenia, kama ilivyoandikwa katika kitabu cha Ufunuo sura ya 22 nusu ya pili ya msitari wa 20 “na uje, Bwana Yesu.